



MASENO UNIVERSITY
UNIVERSITY EXAMINATIONS 2016/2017

**SECOND SESSION EXAMINATION FOR THE
POSTGRADUATE DIPLOMA IN EDUCATION WITH
INFORMATION TECHNOLOGY**

CITY CAMPUS – SCHOOL BASED

**ECT 519: MBINU MAHSUSI ZA KUFUNDISHA LUGHA
YA KISWAHILI**

Date: 19th December, 2016

Time: 11.00 - 2.00pm

MAAGIZO:

- Swali la kwanza ni la LAZIMA. Jibu maswali mengine matatu.

SWALI LA TANO

- a) Fafanua vigezo utakavyozingatia unapoteua malighafi au vielelezo vya kufunzia darasani mwako. (Alama 5)
- b) Eleza namna unavyoweza kufundisha msamiati. (Alama 5)

SWALI LA SITA

- a) Eleza sababu yako ya kuvienzi vitabu vilivyoteuliwa na Tume ya Elimu na vinginevyo kama ala ya kufunzia lugha na fasihi ya Kiswahili. (Alama 5)
- b) Fafanua matatizo yanayokumba ufunzaji wa lugha na fasihi katika shule za upili nchini Kenya. (Alama 5)

SWALI LA KWANZA

- a) Fafanua jinsi utakavyowaelekeza wanafunzi wako katika somo la ufahamu. (Alama 5)
- b) Eleza jinsi utakavyowakwamua wanafunzi wako walioathiriwa na lugha ya kwanza unapofunza lugha na fasihi ya Kiswahili. (Alama 5)
- c) Fafanua namna utakavyowamakinisha wanafunzi ili kuchangamkia makala ya ufahamu yatakayosomwa darasani. (Alama 5)
- d) Thibitisha wazo kuwa 'Haifai kufunza bila kuongozwa na taarifa ya somo.' (Alama 5)
- e) Eleza matatizo unayoweza kukumbana nayo unapofunza ufahamu sikizi darasani mwako. (Alama 5)
- f) Huku ukitoa mifano, eleza njia utakazotumia kufaulisha mafunzo ya insha katika vidato vya chini na vya juu. (Alama 5)

SWALI LA PILI

- a) Mwongozo wa usahihishaji wa insha humwezesha mwalimu kumulika mambo kadhaa ambayo humfaidi yeye na mwanafunzi wake. Fafanua tathmini hii. (Alama 10)

SWALI LA TATU

- a) Jadili jinsi utakavyotumia mbinu mseto katika kufunza lugha na fasihi ya Kiswahili darasani mwako. (Alama 5)
- b) Fafanua umuhimu wa mbinu mseto katika ufunzaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili. (Alama 5)

SWALI LA NNE

- a) 'Wanafunzi wengi hawapendelei somo la ushairi.' Thibitisha kauli hii. (Alama 5)
- b) Fafanua njia tano utakazotumia kuwahimiza wanafunzi wako kupenda kusoma mashairi. (Alama 5)